

## 13J-Hitimisho Kuhusu Al-Waqfu Wal-Ibtidaai (Kisimamo Na Kianzio):

Hitimisho Kuhusu الْوَقْفُ وَالْإِبْتِدَاءِ Al-Waqfu Wal-Ibtidaai (Kisimamo Na Kianzio):

Wanavyuoni wamekubaliana yafuatayo kuhusiana na somo hili la الْوَقْفُ وَالْإِبْتِدَاءِ Al-Waqfu wal-Ibtidaai (Kisimamo na Kianzio):

1. Kusimama katika mwisho wa Aayah ni Sunnah iliyothibiti kwa Mtume (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ):
2. Hakuna katika Qur-aan kisimamo cha kuwajibika au cha haraam isipokuwa kile kinachoharibu maana.

Kwa mwanafunzi wa kawaida anayetaka kujisalimisha na kosa la kusimama katika neno litakaloharibu au kupotosha maana iliyokusudiwa, anaweza kusimama popote apendapo katika alama zozote za Qur-aan isipokuwa tu asisimame katika alama ya ﷺ. Na pia asisimame katikati ambako hakuna alama yoyote kwa sababu aghlabu kusimama kwenye neno lisokuwa na alama huenda ikawa ni 'Kisimamo Kinachochukiza' kutokana na upungufu katika uhusiano baina ya maneno mawili kimaana na kilugha na hivyo hata kuanzia kwake neno la pili likawa ni kosa kubwa katika kuanzia kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى). Mifano:

1. Kusimama katika neno: وَتَسْبِحُوهُ katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

لِتُؤْمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَتُعَزِّزُوهُ وَتُوَقِّرُوهُ وَتَسْبِحُوهُ بُكْرَةً وَأَصِيلًا<sup>①</sup>

((Ili [nyinyi] mumwamini Allaah na Rasuli Wake, na mumsaidie na mumheshimu (Mtume Muhammad (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ) na mumsabbih (Allaah (سبحانه وتعالى) asubuhi na jioni.))<sup>1</sup>

---

<sup>1</sup> Al-Fat-h (48: 9)

Kwa sababu atakaposimama kwenye neno hilo, huenda ikafahamika kwamba kitendo hicho cha “kusabbih” (kumtakasa Allaah) kinaungana na viwili vilotajwa nyuma yake vya ‘kumsaidia na kumheshimu Mtume ﷺ na hali hapo maana ya “kusabbih” inamrudia Allaah (سبحانه وتعالى) Ambaye Ameanzwa kutajwa katika Aayah.

2. Kusimama katika neno: ﴿لَا تُشْرِكُ بِاللَّهِ﴾ katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿وَإِذْ قَالَ لُقْمَانُ لَأَبْنِيهِ وَهُوَ يَعْظِهُ رَبِّنِي لَا تُشْرِكُ بِاللَّهِ إِنَّ الْشَّرِكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ﴾

((Na [kumbusha pale] Luqmaan alipomwambia mwanawe huku akimuwaidhi: “Ee mwanangu! Usimshirikishe Allaah, hakika shirki ni dhulma kubwa mno!”))<sup>2</sup>

Kwa sababu ikisimamiwa neno hilo na kuanziwa linalofuatia: ﴿بِاللَّهِ﴾

Italeta maana kwamba msomaji anaanza kuapia kwa jina la Allaah ﴿لَا تُشْرِكُ بِاللَّهِ﴾ na hali lilokusudiwa ni: (سبحانه وتعالى) (Usimshirikishe Allaah)

Hiyo ni mifano miwili mionganini mwa mingi, na pindi msomaji atakaposimamia neno ambalo halikuwekewa alama basi ni vyema arudie maneno ya nyuma ili aunganishe na yanayofuatia hadi afikie kwenye alama inayoruhusu kusimama.

---

<sup>2</sup> Luqmaan (31: 13)